# SHULE YA SEKONDARI NAMWAI

S.L.P 174, SANYA JUU – SIHA

SIMU: +255 688 154 873

Barua pepe: namwaisecondary@gmail.com


Kumb. Na. NSS/JIF/2007/15. 15/12/2020

**MZAZI/MLEZI WA**.............................................................................................

## YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YA SEKONDARI NAMWAI-2021

Ninayo furaha kukujulisha kuwa mwanao..............................................................amechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza kwa mwaka wa masomo **2021** katika shule ya sekondari Namwai. Hivyo ukiwa mzazi/mlezi wa mwanafunzi husika unapaswa kuwajibika ipasavyo katika kutekeleza maagizo yote ya shule kwa hekima, utii na uaminifu.

## MAAGIZO YA SHULE

Shule itafunguliwa rasmi tarehe **11/01/2021** na mwanafunzi anatakiwa kuwepo shuleni siku hiyo bila kukosa saa 1.00 Asubuhi.

### 1. SARE ZA SHULE

Sare ya Shule yetu ni suruali za marinda 2 kwa wanafunzi wa kiume na sketi mbili za rinda boksi kwa wanafunzi wa kike zote hizo za rangi ya dark blue, shati nyeupe za tetroni mikono mifupi, sweta rangi ya dark blue, tisheti dark blue, viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba na visigino vifupi na soksi nyeusi kwa wanafunzi wa kiume na nyeupe kwa wanafunzi wa kike. Jedwali lifuatalo linaonesha mchanganuo wa sare kwa kila mwanafunzi wa kiume/ kike.

| Jinsi | Suruali/sketi | Shati | Sweta | Viatu(pea) | Tisheti | Soksi (pea) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| wavulana | 2 | 2 | 1 | 2 | 1 | 2 |
| wasichana | 2 | 2 | 1 | 2 | 1 | 2 |

## 2.MAHITAJI YA DARASANI

Kila mwanafunzi anatakiwa awe na counter Book(Quire 3) 11 kwa ajili ya masomo ya darasani, daftari ndogo 11 kwa ajili ya mazoezi ya kila wiki,Dictionary (Oxford) moja, mkebe wa hisabati wenye vifaa vyote, kalamu za kutosha, penseli na ufutio.

## 3. SHERIA,TARATIBU NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria Na 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyofanyiwa marekebisho kwa sheria Na 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo inayotolewa na wizara ya elimu sayansi na teknolojia yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu. Mwanafunzi atatakiwa kuzingatia mambo muhimu yanayofafanuliwa kwa maandishi na atapewa nakala yake mara atakaporipoti shuleni.

(i).Kuwa na heshima kwa walimu,viongozi,wazazi,wafanyakazi wote wa shule, wanafunzi wenzako na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima

(ii).Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima

(iii).Ni lazima kila mwanafunzi kushiriki shughuli za jioni atakazopangiwa.

(iv).Kuwahi shuleni kila siku za masomo saa 1.00 asubuhi pamoja na kufika kwa wakati kwenye shughuli mbalimbali atakazopangiwa awapo shuleni

(v).Kuvaa sare za shule kila atakapokuwa eneo la shule na kwenye ziara mbalimbali za kitaaluma

(vi).Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

(vii)Kutunza mali za shule

(viii)Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira kwa ujumla.

(ix)Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote .

## 4.MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA MASOMO.

(i).Wizi

(ii).Uasherati

(iii).Ubakaji

(iv)Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi nk.

(v).Kupigana na kupiga.

(vi). Kuharibu kwa makusudi mali ya umma

(vii).Kudharau bendera ya Taifa.

(viii).Kupata mimba/kusababisha mimba

(ix).Kuoa au kuolewa.

(x).kutoa mimba.

(xi).Kugoma au kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule.

(xii).Kukataa adhabu kwa makusudi

(xiii) kumiliki simu ya mkononi.

**5. MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI**

**(i)**. Medical Examination form ambayo imejazwa na mganga mkuu wa Wilaya. Form hii ikabidhiwe kwa mkuu wa shule mara mwanafunzi atakaporipoti shuleni.

(ii). Form ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai

(iii). Form ya mzazi/mlezi kukiri kumtimizia mtoto wake mahitaji muhimu.

**MUHIMU**: Tafadhali soma kwa makini maelekezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**HONGERA NA KARIBU SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI NAMWAI**

**ANNA JOSEPH URASSA.**

**MKUU WA SHULE**

**Mawasiliano: 0688154873**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI NAMWAI

**7. AHADI NA UTHIBITISHO WA MZAZI/MLEZI KUMTIMIZIA MTOTO WAKE MAHITAJI YA SHULE**

Mimi.......................................................................................................mzazi/mlezi
wa...........................................................................aliyechaguliwa kujiunga kidato cha ........ nathibitisha kuwa nitamtimizia mtoto wangu mahitaji yake yote kwa wakati.

Sahihi...................................................................................................Tarehe...........................................................

**8. AHADI YA MWANAFUNZI KUTII SHERIA ZA SHULE NA KUTOSHIRIKI KATIKA MIGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI.**

Mimi............................................................................................................ninaahidi kuwa nitatii sheria za shule na pia sitashiriki au kuongoza mgomo au kujihusisha na kitendo chochote kitakachopelekea uvunjifu wa amani hapa shuleni.

Sahihi....................................... Tarehe.........................

**9. TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI.**

(i) Jina kamili la mwanafunzi.........................................................................................................

(ii) Tarehe ya kuzaliwa...................................................Kabila.........................................................

(iii) Jina la mzazi/mlezi............................................................kazi yake................................................

Anapofanyia kazi...........................................................namba yake ya simu................................

**10.TAARIFA YA KUBAINI WATOTO YATIMA.**

**Weka alama ya vema (V) panapohusika**

(i).Baba yupo, mama alishafariki ( )

(ii).Mama yupo, Baba ameshafariki ( )

(iii). Baba na Mama wote walishafariki ( )

**MUHIMU**: Fomu hii ijazwe kikamilifu na kuwasilishwa ofisi ya mkuu wa shule siku ya kuripoti .

## NAMWAI SECONDARY SCHOOL

## MEDICAL EXAMINATION FORM

TO BE COMPLITED BY A MEDICAL OFFICER

NAME OF STUDENT.......................................................................................FORM......................

BLOOD COUNT (Red and White)...................................................................................

STOOL EXAMINATION...........................................................................................................

URINE ANALYSIS.................................................................................................................

STAPHILIA TEST...................................................................................................................

TB TEST.................................................................................................................................

EYES TEST.............................................................................................................................

EARS TEST...........................................................................................................................

CHEST...................................................................................................................................

SPLEEN ................................................................................................................................

ABDOMEN...........................................................................................................................

ADDITIONAL INFORMATION eg. Physical defects of impairments........................................

..............................................................................................................................................

Infections, chronic or family diseases.......................................................................................

Please certify that the above is fit/not fit to enrolled at NAMWAI SECONDARY SCHOOL

NAME..........................................................................SIGNATURE...................................

DESIGNATION.....................................................................STATION.......................................

DATE.........................................................

NB: To medical officer.At the time of examination, please **TREAT** The individual for any ailment you note.